

PAC yapongeza eGA kusimika mifumo ya TEHAMA serikalini

Na Augusta Njoji, DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imepongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kwa kuokoa fedha nydingi za serikali zilizokuwa zinatumi-ka kununua mifumo ya TEHA-MA nje ya nchi.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Japhet Hasunga, alitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki baada ya kamati hiyo kutembelea Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGOVRIDC) cha mamlaka hiyo jijini hapa.

"Kamati yetu imefurahi, tume-fundishwa kuangalia mabaya na ndio tumefundishwa hivyo, na kuyasemea madhaiju lakini katika hili tuwaongeze mmewez-esha serikali kuokoa fedha ny-

ingi kwa kusanifu na kutengeza mifumo ya TEHAMA inayotumi-ka katika taasisi mbalimbali za umma ambayo hapo awali mifumo hiyo ilinunuliwa kutoka nje ya Tanzania kwa gharama kubwa," alisema.

Hasunga alisema taasisi mbalimbali za umma walizozitem-belea siku za nyuma zilikuwa na tatizo la mifumo ya Tehama, lakini kwa sasa zimeimarika kuto-kana na kazi iliyoanywa na eGA.

"Moja ya jambo lililokuwa li-natusumbua sana kamati hii ni taasisi nydingi kununua mifumo ya TEHAMA kutoka nje, lakini msimbo (source code) unabaki kule kwa waliotengeneza mifumo na wakati mwengine mifumo hiyo baada ya muda haitumiki tena na hivyo sisi tumekuwa tu-

nasema hakuna thamani ya fedha katika ununuaji mifumo hiyo ambayo tumetumia gharama kubwa sana kuinunua.

"Kuna taasisi zilinunua mi-fumo kwa zaidi ya Sh. bilioni 30, lakini mfumo haujamaliza mwa-ka wanautupa na tulipowauli-za walisema waliona mfumo huo haufai, hivyo wameamua kutafuta mfumo mwengine. Sisi tunasema hakukuwa na thamani ya fedha," alisema.

Alitaka mamlaka hiyo ku-hakikisha taasisi nydingi zaidi zinaunganishwa katika Mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa Seri-kalini (GovESB), ili kurahisisha upatikanaji huduma za serikali mtandao kwa wananchi.

"Tumefurahi sana kuona namna mifumo mbalimbali inavyowasiliana, tujitahidi tufike

angalau asilimia 80 tu tutakuwa tumefika pazuri kwa sababu tutapunguza gharama na malalamiko katika utoaji hu-duma za serikali mtandao," alisema.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Me-nejimenti Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, alisema kituo hicho kwa sasa kinakibiliwa na ufinyu wa eneo, hivyo eGA inahitaji kutengewa bajeti ili kujenga mi-undombinu (majengo) yake katika eneo la Kikombo.

Awali Mkurugenzi Mkuu wa eGA, Benedict Ndomba, alishukuru kamati hiyo kutembelea kituo hicho na kuahidi kutekeleza maelekezo, maoni na ushauri uli-tolewa na wajumbe wa kamati hiyo ili kuimarisha ubunifu na utafiti wa serikali mtandao.